



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MAHAFALI YA 11 YA KITAALUMA KWA WAUGUZI NA WAKUNGA.**

**Dodoma; 05.04.2024**

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, anawataarifu Wahitimu wote wa kozi za Uuguzi na Ukunga waliofaulu Mtihani wa Usajili na Leseni uliofanyika tarehe **16.02.2024** kuwa, Mahafali ya kumi na moja ya kitaaluma ya kutunuku Vyeti vya Usajili na Leseni, yanatarajiwa kufanyika siku ya Alhamisi tarehe **18.04.2024** kuanzia saa **01:00 Asubuhi** katika ukumbi wa **“CATHEDRAL SOCIAL HALL”** Jijini - Dodoma ambapo mada mbalimbali zitatolewa kisha kiapo.

**Maelekezo ya kufika Ukumbini;** Ukumbi upo Mkabala na Jimbo Kuu la Kanisa Katoliki-Dodoma, Barabara inayotokea usawa wa geti la Bima la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, kuelekea lango Kuu la Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe.

Washiriki wote mnatakiwa kuthibitisha Ushiriki wenu kwa kujaza fomu ya Mahafali kupitia **TOVUTI** ya Baraza la Uuguzi na Ukunga [www.tnmc.go.tz](http://www.tnmc.go.tz).

Aidha, washiriki wote mnaelekezwa kuwa, mnatakiwa kuvaa Sare ya Kitaaluma **“Professional Uniform”** iliyoidhinishwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga kama ifuatavyo: -

1. **WANAWAKE-** Magauni au Suruali na Blauzi rangi nyeupe ndefu.
2. **WANAUME-** Kaunda suti- Shati jeupe na suruali dark blue
3. **VIATU-** Vinavyofunika miguu na siyo vya wazi, viwe vya rangi nyeusi, nyeupe au brown.
4. Kitambulisho cha NIDA, Mpiga kura, Indexing Card au cha kazi kwa wale walioajiriwa.

**NB: Sandozi au Kandambili haviruhusiwi.**

Kwa mawasiliano zaidi piga namba 0682896529,0622958841 na 0762003800

**Imetolewa na;**

**Ndimmyake Mwakapiso  
Afisa Uhusiano na Mawasiliano**